

# MUDA WA MABADILIKO: KUANZA SHULE VIZURI

## Fomu ya maelezo kwa familia

**Wakati wewe na mtoto wako mnatulia mwanzoni wa mwaka huu, mtoto kuanza shule ya msingi huonekana kuwa muda mrefu hapo mbeleni. Kuanza shule kunawezekana kuwa changamoto pamoja na kutamanishwa, na fomu hii ya maelezo inatoa maoni kadhaa jinsi elimu ya sasa ya mtoto wako itakavyosaidia wewe na mtoto wako anapolenga kuingia shuleni wakati mwaka huu unapoendelea.**

Mtoto wako tayari amepata mabadiliko madogo na makubwa katika maisha yake. Jinsi mtoto wako anavyomudu mazingira mapya (kwa mfano, mnapokwenda likizoni, anapoanza *child care* (utunzaji wa mtoto mchanga) au chekechea (*kindergarten*), kucheza na wenzake nyumbani mwao, au hata kupitia mabadiliko mbalimbali ya kila siku) inaleta picha ya jinsi mtoto wako anavyomudu mambo mapya na jinsi anavyoweza kusaidiwa nyakati hizi.

### KWA NINI NI MUHIMU KUANZA SHULE VIZURI?

Kuanza shule vizuri kunaleta matokeo mazuri zaidi kwa mtoto wako kama kujifunza vizuri zaidi na kutulia vizuri zaidi anapopata mabadiliko mwanzoni na baadaye. Inasaidia mtoto wako kwamba elimu na maendeleo yake yaende mfululizo, na kujisikia kutunzwa, kutosikia wasiwasi na kuzoea watu wapya na mahali panya.

### KUSAJILISHA MTOTO WAKO SHULENI

Idadi kubwa zaidi ya shule za msingi zinaanza usajili katika mwezi wa 5 wa mwaka ule kabla ya mtoto kuanza shule. Unapomsajilisha mtoto wako, waweza kujua zaidi kuhusu shule ile kwa kushiriki mipango na shughuli zinazohusu muda huo wa mabadiliko. Kwa kusaidiwa zaidi kwenye muda huo wa mabadiliko ni afadhali muda uanze siku nyingi kabla ya mwisho wa mwaka na kuendelea siku nyingi baada ya siku zile za kwanza za shule.

### KUANZA KUSHIRIKI MIPANGO NA SHUGHULI YA SHULE

Mkishiriki katika mipango na shughuli za shule, wewe na mtoto wako mtasaidiwa zaidi kuelewa shule itakavyokuwa

na kuanza kuwafahamu watoto wengine na familia zao ambao watakuwa wanahudhuria shule hiyo.

### HABARI KUHUSU ELIMU NA MAENDELEO MUDA HUU WA MABADILIKO

Mwalimu ambaye anamfundisha mtoto wako kwa sasa ataandika *Transition Learning and Development Statement* (Taarifa ya Mpito yaani Habari ya Elimu na Maendeleo wakati wa Mabadiliko). Fomu hii itasema kwa kifupi kuhusu shauku, vipawa na uwezo wa mtoto wako. Pia itaonesha njia na mikakati (maarifa) ya elimu ya pekee, ili shule ya mtoto wako na mwalimu wa prep wataweza kumzoea mtoto wako upesi na kumpangia mipango ya kufaa ya kumfundisha.

Ikiwa utakusudia kumtuma mtoto wako kwa *Outside School Hours Care* (Huduma ya Utunzaji wa Muda Nje ya Masaa ya Vipindi), fomu ya Taarifa ya Mpito inaweza kushirikishwa na huduma hiyo pia. Fomu hii inasaidia watunzaji wa *Outside School Hours Care* (Huduma ya Utunzaji wa Muda Nje ya Masaa ya Vipindi) kumpangia mtoto wako kufuatana na shauku zake na kumtegemeza katika mfululizo wa utoto, shule na *Outside School Hours Care*.

Taarifa ya Mpito inaweza kukusaidia kufahamu, kutegemeza, kuwasiliana na kutetea elimu ya mtoto wako wakati anapoingia shule. Wewe mwenyewe utapata nakala kamili ya Taarifa ya Mpito ya mtoto wako.

Katika Taarifa ya Mpito ya mtoto wako kuna maelezo kuhusu mtoto wako, pamoja na jina lake, tarehe ya kuzaliwa na picha; pia jina lako lipo na anwani na namba za simu. Ikiwa inahusika, fomu itaarifu jina na anwani na simu ya wale wengine ambao kwa sasa wanategemeza mtoto wako.

Kwa kawaida, Taarifa ya Mpito hujazwa katika Muhula wa 4, lakini ikiwa mtoto wako amelemaa au haendelei kama kawaida, wale wanaomtumza au kumfundisha sasa waweza kuandika *Taarifa ya Mpito* mapema kama katika mwezi wa 6 au wa 7, ili kuanzisha mazungumzo nawe na shule iliyochaguliwa kuhusu misaada ambayo atahitaji.

Kwa sababu wewe wajua mengi kuhusu mtoto wako, mchango wako ndani ya fomu ni ya maana sana. Utakaribishwa kujaza sehemu ya Taarifa ya Mpito. Kujaza sehemu hiyo kutasaidia shule kuanza kujua jinsi watakavyoweza kukusaidia wewe na mtoto wako ili nyote mweze kushirikiana na muda mzuri wa kuanza shule.

Tena, kuna sehemu kwa mtoto wako kujaza (pamoja na msaada wa mtu mzima, ama wewe au mwalimu wa muda huo wa sasa). Kipengele hiki kwa kawaida kina nafasi kwa picha na kinaarifu yale ambayo mtoto wako anavutwa nayo na pia mawazo yake kuhusu shule na kuianza.

### JINSI MAELEZO HUSHIRIKISHWA NA SHULE YA MTOTO WAKO

Kuanzia 2018, Taarifa ya Mpito itakamilishwa, kushirikishwa na kutunzwa kwa njia ya interneti kwenye tovuti iliyoitwa *Insight Assessment Platform* (tovuti yenye misaada ya vipimo vya elimu pamoja na maendeleo). Taarifa zote zilizo kwenye *Insight Assessment Platform* hutunzwa kwa uangalifu humu nchini Australia.

*Insight Assessment Platform* hiyo tayari inatumika katika shule zote za serikali ya Victoria na inawezesha shule kutunga taarifa ya kudumu ya elimu na maendeleo ya mtoto wako. Baadhi ya shule za Kikatoliki na shule za binafsi zaweza kupata Taarifa ya Mpito ya mtoto wako kwa njia ya *Insight Assessment Platform* au zitapokea nakala ya kikaratasi au ya interneti toka kwa wale wanaomfundisha mtoto wako sasa.

Idara ya Elimu na Mafunzo huwaajiri watoaji huduma wengine ili kusaidia baadhi ya kazi zake. Wakati inapofanya hivi, Idara huhakikisha kuwa siri zote zinatunzwa kama ilivyo kawaida yake. Pia, Idara imefanya makadirio ya utunzaji wa siri katika tovuti ya *Insight Assessment Platform*, ili kuhakikisha kuwa utunzaji huo ni sahihi kufuatana na Sera Zinazohusu Utunzaji wa Taarifa ya Idara, na Sheria zingine kuhusu kutunza siri.  
[www.education.vic.gov.au/Pages/privacypolicy](http://www.education.vic.gov.au/Pages/privacypolicy).

Taarifa kutoka kwa Taarifa ya Mpito hizo na taarifa za usajili toka kwa shule kadhaa zinaweza kutumika na Idara kwa ajili ya kufuatiliwa na kufanywa utafiti. Taarifa hizo zingetunzwa kwa namba na grafu. Majina ya watoto **hayataonekana**.

Kwa maelezo zaidi kuhusu *Insight Assessment Platform* wasiliana na Idara ya Elimu na Mafunzo kwenye [psts@edumail.vic.gov.au](mailto:psts@edumail.vic.gov.au).

### KWA MAELEZO ZAIDI

Tafadhali angalia  
[www.education.vic.gov.au/transitiontoschool](http://www.education.vic.gov.au/transitiontoschool)

Hati hii imetafsiriwa katika lugha mbalimbali ambazo zinapatikana kwenye  
[www.education.vic.gov.au/transitiontoschool](http://www.education.vic.gov.au/transitiontoschool).